



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA



Unapojuibu tafadhali jibu
Kumb.NaKDC/M.1/119/204

UTANGULIZI:

Kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kilizinduliwa rasmi na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati Dr John Pombe Joseph Magufuli mwezi Februari 2020. Hata hivyo utekelezaji ngazi ya kijiji/ mtaa haukuanza mara moja kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya korona. Utekelezaji wa Mpango ulianza rasmi mwezi Julai 2020 kwa kufanya zoezi la uhakiki wa kaya za walengwa kwenye vijiji 75 vilivyokuwa kwenye Mpango.

UTEKELEZAJI

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Halmshauri ya Wilaya ya Kyela imepokea shilingi 937,532,826.00 kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa kaya za walengwa 6,601 katika vijiji 111 (vijiji 93 na kata/vitongoji vya mamlaka ya mji mdogo wa Kyela) kwa walengwa wanaopokea kwa nji ya taslimu kama ifutavyo:

Dirisha la Julai/Agosti na Sept/Oktoba 2021	shs 336,289,412.00
Dirisha la Nov/Des 2021 na Jan/Feb 2022.....	shs 411,458,926.00
Dirisha la Machi/April 2022.....	shs 189,784,488.00
Jumla	shs 937,532,826.00

MAFANIKIO YA MPANGO

Mafanikio kadhaa yamepatikana katika kaya za walengwa kutokana na utekelezaji wa mpango ambapo kaya 418 zimeanzisha biashara ndogondogo za uuza ji wa mbogamboga, matunda,maharage , mawese, maziwa nk. Kaya 928 zimeanzisha ufugaji wa kuku, bata, nguruwe ng'ombe na mbuzi. Kaya 364 zimeboresha makazi kwa kujenga nyumba za tofali na kuezeka/ kulaza bati, kaya 336 zimejenga vyoo vya kudumu.

CHANGAMOTO

1. Baadhi ya walengwa kutokuwa na vitambulisho/namba za NIDA kwa ajili ya kujisajili kwenye malipo kwa njia ya mtandao

UTATUZI WA CHANGAMOTO

1. Kuendelea kuhamasisha walengwa kufuatilia vitambulisho /namba za NIDA

.....
EZEKIEL H. MAGEHEMA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KYELA

Halmashuri ya Wilaya ya Kyela, S. L. P. 320, Kyela, Mbeya , Simu. 025-2540035/7, Nukshi 025-2540425, www.kyeladc.go.tz